

## Ushauri wa COVID-19 kwa familia Shughuli za shule katika \*Greater Sydney

Idara ya Elimu ya NSW na Afya ya NSW zinafanya kazi pamoja kujibu COVID-19.

Kufuatia ushauri kutoka kwa Afya ya NSW masomo kutoka nyumbani yapo kwa shule katika \*Greater Sydney (ikiwa ni pamoja na Blue Mountains, Central Coast, Wollongong na Shellharbour). Shule zipo wazi kwa wanafunzi wote wanaozihitaji. Ikiwa mwanafunzi au mzazi au mtoto ana dalili hata kidogo sana za ugonjwa wa COVID-19 ([COVID-19 symptoms](#)) hapaswi kuhudhuria shule na hapaswi kurudi shuleni hadi atakapokuwa na majibu hasi ya kipimo na hana dalili.

### Barakoa (mask) na vifuniko vya uso

Wakati watu wapo shuleni barakoa/mask ama vifuniko vya uso vinahitajika katika mipangilio yote ya ndani kwa:

- wanafunzi wote katika Mwaka 7 na juu
- wafanyakazi wote.

Misamaha fulani inatumika kwa sheria hizi. Tafadhali rejelea Kanuni za barakoa/mask za uso kwenye tovuti ya Serikali ya NSW ([Face mask rules on the NSW Government website](#)) kwa maelezo zaidi.

### Wageni

Wageni wasio wa muhimu hawaruhusiwi kwenye maeneo ya shule.

Wazazi na walezi lazima wafuate ushauri wa shule yao kuhusu mabadiliko ya kushusha na kuchukua kwa mwanafunzi. Hii ni pamoja na kukaa ndani ya gari wakati wa kushusha na kuchukua watoto ikiwa ni salama kufanya hivyo. Hii haitumiki kushusha na kuchukua watoto kutoka Huduma ya Nje ya Masaa ya Shule (Out of School Hours Care (OOSHC)) kwa sababu utaratibu wa kuingia na kutoka unahitajika.

Wazazi wanapaswa:

- Kufuata ushauri wa umbali wa kimwili kwa eneo lao na epuka kukusanyika pamoja nje ya milango ya shule
- kukaa nje ya viwanja vya shule – mambo mengine ya pekee yanaweza kutumika juu ya Shule kwa Madhumuni Maalum (Schools for Specific Purposes (SSP)), wanafunzi wenye hali ngumu au wanafunzi wenye ulemavu
- kufuata mahitaji ya kuvaa barakoa (mask) na kuingia kwa kutumia Service NSW QR code wakati wanapoingia shuleni.

### Wanafunzi wa HSC

Wanafunzi wa HSC watasaidiwa kuhudhuria shule ili kufanya kazi ya kozi, kazi ya mradi na maandalizi ya mitihani ambapo hiyo haiwezi kufanyikiwa pale nyumbani. Wanafunzi wanaohudhuria watatakiwa kutii kanuni kali za COVID.

### Huduma ya Mkalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi tafadhali upigie simu mkuu wa shule yako. Kama unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako tafadhali pigia simu Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na omba kwa mkalimani katika lugha yako. Hutatozwa kwa huduma hii.